



**TAMKO KULAANI KUKAMATWA KWA VIONGOZI WA CHADEMA,
MAWAKILI, WAANDISHI WA HABARI NA WANAHARAKATI KUELEKEA
SIKU YA VIJANA DUNIANI**

Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC) unalaani kukamatwa kwa Wakili Tundu Lissu ambaye pia ni Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa, Katibu Mkuu wa CHADEMA Mhe. John Mnyika, Mwenyekiti wa CHADEMA Kanda ya Nyasa Mhe. Joseph Mbilinyi, Wakili Deogratias Mahinyila, waandishi wa habari wa Jambo Tv Ramadhan Khamis na Fadhil Kirundwa, wanaharakati na viongozi wa BAVICHA akiwemo Twaha Mwaipaya, Moza Ally, Deusdedith Soka na wengine wengi kwa idadi isiyo rasmi inayokadiriwa kuwa watu zaidi ya 300 wamekamatwa kwa tuhuma ambazo hazijawekwa wazi na Jeshi la Polisi Tanzania.

Deusdedith Soka na vijana wenzake wasiopungua 10 walikamatwa Agosti 10, 2024 majira ya saa mbili usiku wakiwa ndani ya ofisi za CHADEMA Wilaya ya Temeke na kupelekwa kwenye vituo mbalimbali vya Polisi ikiwemo Chang'ombe, Kilwa road na Kigamboni kwa tuhuma za kufanya kusanyiko lisilo halali ndani ya ofisi ya chama chao. Wanaharakati hawa walikamatwa wakiwa wanasubili gari kuelekea Mbeya kwenye maadhimisho ya siku ya vijana duniani.

Katika nyakati tofauti tofauti mnamo Agosti 11, 2024 wanaharakati na vijana waliokuwa wakisafiri kwenda jijini Mbeya kwaajili ya maadhimisho ya siku ya vijana duniani yaliyoan daliwa na Baraza la Viajama Chadema walikamatwa ndani ya magari yao waliyokuwa wamekodi na kufanyiwa upekuzi katika maeneo ya Mikese Morogoro (takribani watu 80), Iringa (takribani watu 90), Makambako (takribani watu 70) na Mbeya (takribani watu 100).

Majira ya jioni Wakili Tundu Lissu (Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa), Katibu Mkuu wa CHADEMA Mhe. John Mnyika, Mwenyekiti wa CHADEMA Kanda ya Nyasa Mhe. Joseph Mbilinyi na viongozi wengine walikamatwa na kupelekwa vituo tofauti tofauti vya Polisi katika jiji la Mbeya. Sisi tunaamini kwamba kukamatwa kwao kuna lenga kuwazuia kufanya shughuli ya maadhimisho ya vijana duniani Agosti 12 jijini Mbeya.

Ibara ya 18 na 20(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zinatoa haki na uhuru wa watu kujumuika, kufanya mikutano, maadhimisho na kueleza mawazo yao. Haki hizi hazipo kwenye Katiba peke yake bali zipo kwenye Mikataba mbalimbali ya Kimataifa na Kikanda ambayo Tanzania imeridhia.

THRDC imesikitishwa na ukiukwaji huu wa Katiba na ukamatwaji huu unaoendelea unafifisha uhalisia wa maridhiano, ustahimilivu na mabadiliko ambayo Mhe. Samia Suluhu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alikuwa akihubili tangu alipoingia madarakani (4Rs: Reconciliation, Resilience, Reforms and Rebuilding). Vijana wanahaki ya kukusanyika na kuadhimisha siku yao duniani, kitendo cha kuwazuia kwa kuwakamata kinaweza kuhatarisha zaidi amani ya nchi kwasababu wanaweza kutumia njia zingine kueleza hisia zao na kusababisha madhara makubwa.

Tunatoa wito kwa Mkuu wa Jeshi la Polisi Nchini kuwaachilia huru watu wote waliokamatwa bila masharti ili waweze kuadhimisha siku ya vijana duniani kama ambavyo vyama vingine tayari vimekwisha adhimisha na hatukuona wakikamatwa.

Pia taarifa ambazo hazijathibitishwa ni kwamba kulikuwa na matumizi ya nguvu wakati wa ukamataji na kupigwa kwa baadhi ya waliokamatwa, kama ni kweli tunalaani suala hili kwani ni kinyume na Katiba, Sheria na taratibu zote za ukamataji.

Tunatoa wito kwa viongozi wengine wa nchi kuanzia Rais wa Tanzania na wengine walione suala hili kuwa linatia doa nchi yetu hivyo wachukue hatua za haraka ikiwa ni pamoja na kuwaagiza Polisi kuwaachia watu wote waliokamatwa ili waendeleo na shughuli zao za maadhimisho ya vijana kama ilivyopangwa kama vile ambavyo Mhe. Rais amekuwa akisisitiza masuala ya demokrasia na 4Rs.

Pia tunawashauri viongozi wa vijana na vijana wote watakaoshiriki katika maadhimisho hayo wazingatie masuala ya utulivu, amani na Sheria za nchi yetu.

THRDC inaendelea kufuatilia suala hili kwa ukaribu sana kwa kushirikiana na mawakili mbalimbali ambao wanafuatilia suala hili kwa ukaribu.

Imetolewa na,

Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania -THRDC

Agosti 12, 2024, Dar es Salaam, Tanzania.